



UJUMBE MUHIMU KWA WAKIMBIZI NA WATAFUTA HIFADHI WOTE WANAOSHISHI MJINI KUHUSU VIRUSI VYA CORONA (COVID-19)

(Iliyotolewa: 27 Aprili 2020)

Mnamo tarehe 15 Machi 2020 serikali ya Kenya ilitangaza hatua maalum za kuzuia kueneza zaidi virusi vya corona (COVID-19). Kutoka tarehe 27 Machi 2020, kuna **amri ya kutotoka majumbani kati ya saa moja jioni mpaka saa kumi na moja asubuhi kila siku kwa watu wote nchini Kenya ambayo kwa hatua hii itaendelea hadi tarehe 16 Mei 2020** (inaweza kuendelea zaidi kulingani na vile hali itakua). Hairuhusiwi kutoka nyumbani mwako wakati huu, au utakamatwa na polisi; ama, unaweza kuwekwa na serikali katika kituo kilichoteuliwa kwa siku 14 kwa gharama yako.

Zaidi ya hayo, mnamo tarehe 6 Aprili 2020, serikali ya Kenya ilitangaza kuwa **hakutakuwa na harakati yoyote ndani au nje ya eneo la jiji la Nairobi kutoka tarehe 6 Aprili 2020 na kaunti za Kilifi, Kwale na Mombasa kutoka tarehe 8 Aprili 2020; vizuizi hivi vitaendelea hadi tarehe 16 Mei 2020**. Zaidi, vizuizi kama hivi vimewekwa kwa **kaunti ya Mandera kutoka tarehe 22 Aprili 2020**. Usijaribu kuingia ndani au nje ya maeneo haya au utakamatwa na polisi. Unaweza kuendelea na harakati zako ndani ya eneo unaloishi.

Unafaa kuvaa maski ya uso ukiwa hadharani – lakini usisahau kunawa mikono yako mara kwa mara kwa sabuni na maji. Hii ni kwa usalama wako na kwa faida yako mwenyewe. Kwa kuongezea, pia utasaidia katika kupunguza kuenea kwa COVID-19. *Lakini ni muhimu kuzingatia:* Usipo vaa maski ya uso, unaweza kutozwa faini ya KES 20,000 na unaweza kukabiliwa na kifungo cha hadi miezi sita au zote mbili.

Ikiwa serikali itafanya **uchunguzi kwa wingi** katika maeneo tofauti kudhibiti kuenea kwa COVID 19 na uko mahali hapo, tafadhali **shirikiana na wafanyikazi kutoka Wizara ya Afya**.

Tafadhali usizunguke sana wakati wa mchana kama sio lazima. Ikiwa ni lazima kuzunguka, unafaa **kubeba vitambulisho vyako vya usajili** kila wakati. Zaidi, **hakikisha unafwatilia** maagizo yanayotolewa na serikali ya Kenya na hakikisha unayafuata.

Nambari za dharura za usaidizi

- **Kwa usajili/dharura za vitambulisho:**
Sekretarieti ya masuala ya wakimbizi Shauri Moyo: 0772057770
- **Nambari ya msaada ya UNHCR:** 0800720063 (bila malipo)
- **Kwa dharura za kiafya:**
NCCK 0704873342 / 0723281352/ 0723281362
- **Kwa dharura za kisheria (kukamatwa, shida na polisi):**
Kituo cha Sheria 0720806531
- **Kwa dharura za riziki:**
Danish Refugee Council 0800720181
- **Kwa masuala yanayohusiana na NHIF (Mfuko wa kitaifa wa bima ya hospitali):**
0740049502
- **Nambari ya ushauri**
1190/ 1199/ 0721 336017
- **Nambari ya GBV**
1195/ 0800720501
- **Nambari ya ulinzi wa mtoto**
116

COVID 19 inaenea moja kwa moja kupitia matone (kukohoa/kupiga chafya) kutoka kwa mtu aliyeambukizwa; moja kwa moja kupitia kuwasiliana na nyuso au vitu vimetumiwa na mtu aliyeambukizwa. Ukiwa na **dalili zozote za COVID-19** kama homa, kikohozi, upungufu wa pumzi na shida ya kupumua, **tafadhali wasiliana na Wizara ya Afya** kupitia 0800721316 (bila malipo); 0732353535; or 0748592558 kwa mwongozo.